

Bibilia ya watoto  
Inawalettea



Mwana wa  
Mfalme Awa  
Mchungaji



Kimeandikwa na: Edward Hughes  
Kimeorodheshwa na: M. Maillot; Lazarus  
Imerekebishwa na: E. Frischbutter; Sarah S;  
Alastair P.

Kimetafsiriwa na: Bethel Children's Home,  
Kisumu, Kenya and Emmanuel Menya  
Kimedhibitishwa na: Bible for Children  
[www.M1914.org](http://www.M1914.org)

BFC  
PO Box 3  
Winnipeg, MB R3C 2G1  
Canada

©2021 Bible for Children, Inc.

License: Kuna ruhusa ya kuchapa hadithi hii, lakini bila ya kuuza.



Siku moja Musa alimuona Mmisri  
akimpiga mtumwa Mwebrania.  
Ingawa Musa alilelewa  
na kuelimishwa kama  
mwana wa Mfalme  
katika ikulu ya Farao,  
yeye pia alikuwa  
Mwebrania.  
Alipaswa  
kumsaidia

huyo mtumwa.




Akiangalia kila upande ili kuhakikisha hakuna anayemtazama, Musa akamshambulia huyo Mmisri katili. Katika mapigano hayo, Musa akamuua Mmisri. Haraka, akauzika mwili wake.



Siku iliyofuata, Musa akaona Waebrania wawili wanapigana. Akajaribu kuwazuia. Mmoja akasema, "Unataka kuniua kama ulivyomuua Mmisri?" Musa akaogopa. Kila mtu alijua kilichotokea jana. Farao alijua. Ilibidi Musa atoroke. Akakimbilia nchi inayoitwa Midiani.



Wakati Musa amepumzika kisimani, mabinti saba wa kuhani wa Midiani wakazijaza birika maji kwa ajili ya kundi la mifugo ya baba yao.




Wachungaji wengine wakajaribu kuwafukuza. Musa akawatetea na kuwasaidia hao wanawake.





Reueli, baba wa wasichana hao akasema kwa mshangao, "Mmerudi nyumbani mapema!" Wasichana walipoelezea sababu ya kuwahi, akasema, "Mleteni huyo mtu hapa." Musa akaishi na Reueli, ambaye jina lake


jingine alitwa Yethro. Baadaye, Musa akamuoa binti mkubwa wa Reueli.





Ikawa Farao huko Misri  
akafa. Watu wa Mungu,  
Waebrania, walikuwa bado  
watumwa. Jinsi gani  
waliugua katika mateso  
yao!

Kiasi gani  
waliomba msaada  
wa Mungu! Mungu  
akasikia maombi yao.



Musa hakujua kinachoendelea, lakini Mungu alipanga kumtumia kusaidia Waebrania waliofanywa watumwa. Miaka arobaini ilikuwa imepita tangu Musa aondoke Misri. Alikuwa mchungaji wa kundi la mifugo ya Reueli. Lakini alikuwa na hamu ya kuwaona



watu wake huko Misri.




Siku moja Musa akaona kichaka  
jirani naye kimeshika moto.  
Lakini ule moto ukawa  
haukiteketezi kichaka.  
Musa akaamua kufuatilia  
sababu yake.



Musa alipokikaribia, Mungu akamuita kutokea kwenye kile kichaka. "Musa!" Musa akasema, "Mimi hapa." Mungu akasema, "Usikaribie mahali hapa." "Vua viatu miguuni pako, kwa sababu mahali uliposimama ni nchi takatifu."



Mungu akasema, "Nitakutuma kwa Farao kuwatoa watu wangu katika Misri." Musa akaogopa kwenda.



Kisha Mungu akamuonyesha Musa uwezo wake mkuu. Akageuza fimbo ya Musa kuwa nyoka.



Musa aliposhika mkia wa nyoka akawa fimbo tena.  
Mungu akampa ishara nyingine.



Akamwamuru, "Tia mkono wako kifuani mwako."  
Musa akafanya hivyo. Mkono wake ukageuka na  
kuwa mweupe wenye ukoma.







Alipoutia tena, mkono wake ukaponywa.



Bado Musa akakataa. Akamwambia Mungu, "Siwezi kusema vizuri." Mungu akakasirika. Akasema, "Nitamtumia Haruni, ndugu yako, kusema maneno utakayomwambia."



Musa akarudi kwa Yethro, akafungasha vitu vyake na kwenda Misri.



Mungu akamuongoza Haruni ndugu yake Musa kukutana na Musa mlimani. Musa akamuambia Haruni mambo yote kuhusu mpango wa Mungu wa kuwaweka huru Waebrania kutoka kwa Wamisri. Kwa pamoja, wakapeleka habari kwa viongozi wa Waebrania.

Musa alipoonyesha ishara kwa wazee wa Waebrania, wakajua Mungu atawasaidia.


Kwa pamoja, wakainama na kuabudu.



Kwa ujasiri, Musa na Haruni wakaenda kwa Farao. Wakamwambia, "Mungu anasema, 'Wape ruhusa watu wangu waondoke.'"



Farao akajibu, "Sitawaruhusu  
waondoke." Hakuwa tayari kumtii  
Mungu. Ilibidi Mungu atumie uwezo  
Wake mkuu kubadili nia ya  
Farao.



Mwana wa Mfalme Awa Mchungaji

Hadithi kutoka kwa Neno la Mungu, Bibilia,

inapatikana katika

Kutoka 2-5

"Kufafanusha maneno yako kwatia nuru."

Zaburi 119:130






Mwisho



10



60





Hii hadithi ya bibilia inatueleza kumhusu Mungu wetu wa ajabu aliyetuumba na anayetaka tumjue.

Mungu anajua tumetenda mambo mabaya, anayoyaita dhambi. Adhabu ya dhambi ni mauti, lakini Mungu anakupenda sana hata akamtuma mwana wake wa pekee, Yesu, Ili afe msalabani na aadhibiwe kwa dhambi yako. Alafu Yesu akafufuka na kuenda nyumbani mbinguni! Ukimwamini Yesu na kumwomba msamaha kwa dhambi yako, Atakusamehe! Yesu atkuja na kuishi ndani yako, na utaishi naye milele.

Kama unaamini huu ni ukweli, Sema haya kwa Mungu: Mpendwa Yesu, ninaamini kuwa wewe ni Mungu, na ulifanyika mtu ili ufe kwa ajili ya dhambi zangu, ili niwe na maisha mapya, na siku moja nitaenda kuwa nawe millele. Nisaidie nikutii na niishi kwa ajili yako kama mtoto wako. Amina.

Soma bibilia na uzungumze na Mungu kila siku! Yohana 3:16

